**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu

*Martin Mulei*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Mountains of the Moon Uganda, S. L. P. 837, Kabarole, Uganda.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: muleim1@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*08 Mei 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Kanuni, Vipashio Vya Kimofosintaksia, Mifanyiko, Athari Za Mwingiliano, Ubia Na Upatanifu.*

**IKISIRI**

Uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia baina ya lugha asili na Kiswahili umeripotiwa kusababisha athari za mwingiliana katika matumizi ya Kiswahili. Luganda na Kiswahili ni lugha za Kibantu ambazo huzingatia kanuni katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia. Lugha hizi za Kibantu, hudhihirisha upekee wa mfumo katika matumizi ya vivumishi kimofosintaksia. Utambuzi wa kanuni za kimofosintaksia ni msingi katika matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Kwa hiyo, makala hii inadhamiria kueleza jinsi kanuni za mifanyiko ya vivumishi vya Luganda hufanana na kutofautiana na za Kiswahili kimatumizi. Kwa kuzingatia mihimili ya Ubia na Upatanifu ya Chomsky (1981), data za matumizi ya kanuni za vivumishi zilikusanywa maktabani kupitia kwa usomaji na uhakiki wa maandishi. Inatarajiwa kuwa utambuzi wa kanuni za mifanyiko ya vivumishi, michango ya kanuni za lugha asili katika ujifunzaji wa Kiswahili, utaweka mikakati ya ujifunzaji ya kuepukana na athari za mwingiliano wa vipashio vya lugha asili katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

**APA CITATION**

Mulei, M. (2023). Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 132-153. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206.

**CHICAGO CITATION**

Mulei, Martin. 2023. "Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 132-153. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206.

**HARVARD CITATION**

Mulei, M. (2023) "Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 132-153. doi: 10.37284/jammk.6.1.1206.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**IEEE CITATION**

M. Mulei, "Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 132-153, May. 2023.

**MLA CITATION**

Mulei, Martin. "Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, May. 2023, pp. 132-153, doi:10.37284/jammk.6.1.1206.

## UTANGULIZI

### Usuli wa Mada

Kanuni za mofosintaksia ni sheria za kiisimu au sarufi zinazoeleza uhusiano uliopo baina ya vipashio vya mofolojia na sintaksia zinazoelekeza na kufafanua usahihi katika matumizi ya lugha. Usahihi hujitokeza katika utungaji wa tungo zenye mantiki unaozingatia viwango vya mofolojia na sintaksia kimaandishi na kimazungumzo. Umantiki hurejelea jinsi vipashio vya mofolojia vinavyoungana na kuhusiana kuunda tungo zenye maana (Barno, 2013; Mulei na wenzake, 2021; Oichoe, 2005). Kimsingi, kivumishi ni neno linaloeleza zaidi kuhusu nomino, kiwakilishi na au kivumishi kingine katika tungo (Mbwillow, 2017). Kwa mujibu wa maelezo haya, kivumishi ni kipashio cha kimofosintaksia ambacho hutumika pamoja na nomino kama viambajengo vya virai nomino, kutoa maelezo zaidi kuhusu nomino kama neno kuu katika tungo virai nomino, vishazi nomino, na vishazi vivumishi (vishazi virejeshi na vishazi vihusishi).

Lugha za nasaba moja huweza kuwiana na kutofautiana kiisimu. Uwiano na tofauti hizi huweza kubainika katika kanuni, aina, maumbo na miundo ambayo hujitokeza katika matumizi. Licha ya kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha za Kibantu zenye nasaba moja, kila lugha imeainishwa kutokana na upekee wa sifa za kiisimu (Mulei na Wenzake (2021). Hii inatokana na kuwa kila lugha ina upekee wa kanuni, muundo na mpangilio wa maneno katika tungo zake (Mbaabu, 1992). Sifa hizi ndizo zinazopambanua na kutofautisha lugha za nasaba moja. Hii ina maana kuwa, Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti kiisimu licha ya kuwa lugha za nasaba moja. Aidha, kaida katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia ni muhimu katika kujenga matumizi bora ya lugha. Makala hii inatokana na sababu kuwa *uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za vipashio vya kimofosintaksia baina ya lugha asili na Kiswahili sanifu huweza kusababisha athari za mwingiliano katika matumizi ya Kiswahili sanifu.* Aidha, utafit huu ulinuia kuchanganua miundo na kanuni za matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu katika tungo, kubainisha kanuni na sheria zinazotawala matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu na Kujadili Uwiano na tofauti za kanuni za mifanyiko ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu.

Kwa hiyo, ni muhimu kuhakiki na kutambua kanuni zinzodhihirika katika matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia vya lugha asili kurahihisha matumizi na kuepukana na athari za mwingiliano wa kanuni za lugha za nasaba moja. Utafiti huu upo katika eneo la kithematiki wa isimu linganishi na tumikizi ambao unachanganua mofosintaksia ya lugha za Kibantu za Luganda na Kiswahili sanifu. Aidha, ulichunguza jinsi isimu ya lugha za Kibantu huchangiana, kuingiliana na kuathiriana katika matumizi ya vipashio vya kiisimu. Makala haya yanaweka wazi uwiano na tofauti za kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Tafiti mbalimbali zimeonyesha kuhusiana na kutofautiana kwa vipashio na kanuni za matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia na changamoto katika matumizi. Baadhi ya kanuni hizi zimeelezwa kuwa bia na husababisha kuwepo kwa miundo mbalimbali ya tungo katika lugha mbalimbali. Mathalani, Kemuma (2022) akibainisha kanuni na

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

sheria zinazotawala muundo wa maneno katika sentensi sahili ya Ekegusii, alitambua kuwa lugha za Ekegusii na Kiswahili miongoni mwa zingine ziliainishwa kama lugha za nasaba moja zenye muundo wa sentensi unoaonekana kufanana katika kipengele cha sintaksia ya upatanifu wa nomino na maneno mengine katika tungo. Alidhihirisha kuwa muundo wa sentensi unahusu mpangilio wa viambajengo katika sentensi. Aidha, muundo wa virai wa sentensi sahili ya Ekegusii hutegemea majopo leksia ya maneno kisarufi kama vile nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi na kihusishi na jopo amilifu.

Kulingana na Massamba na wenzake (1999), lugha za Kibantu hushabihiana kimuundo na kisifa hasa katika muundo wa maneno wa kudhihirisha mfuatano wa viambishi ambao hutokea mwanzoni baada ya mizizi. Obara (2014) akichanganua makosa ya kifonolojia, kimofolojia, na kisintaksia katika insha za wanafunzi wazungumzaji wa Ekegusii, aligundua kuwa wanafunzi ambao lugha ya kwanza (L1) ni Ekegusii walikiuka kanuni ya upatanishi wa kisarufi wakati wanapotumia vivumishi. Katika utafiti wake alibaini kuwa wanafunzi walihamisha na kujumlisha kanuni za kiisimu za L1 katika matumizi ya vipashio vya kiisimu fonimu, muundo wa maneno, virai, vishazi na sentensi za Kiswahili. Kulingana na Obara (keshatajwa), ukiukaji huu ulitokana na tofauti ya fonolojia, sintaksia, miundo ya maneno ya Ekegusii na ile ya Kiswahili sanifu. Aidha, Nicolle (2007) katika kufafanua juu ya vibainishi vionyeshi ambavyo ni vivumishi vionyeshi, anaeleza kufanana na kutofautiana kwa aina za vionyeshi katika lugha za Kibantu. Kiuwiano, anaeleza kuwa katika lugha mbalimbali za Kibantu, viambishi vionyeshi huanza na kiambishi tangulizi, kiambishi awali na mzizi. Katika kutofautiana, anaeleza kuwa aina za vionyeshi si sawa katika lugha zote za Kibantu.

Gibson na Guérois (2019) walielezea kiwango cha mfanano na tofauti katika mofolojia na sintaksia baina ya lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki kutumia vigezo 142 vinavyohusisha sehemu maalumu za mfumo wa sarufi. Matokeo ya ulinganishi wao yalibainisha kwamba, kwa upande mmoja lugha hizi zinafanana kisarufi, lakini kwa upande mwingine zinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Matokeo ya ulinganishi wa lugha za Uganda ulibainisha kwamba lugha za kundi la Kaskazini za Kinyoro (JE11), Kinyole (E35), na Kiganda (JE15), zote zina uhusiano zaidi ya asilimia 70 baina yao kimofolojia na kisintaksia. Utafiti wao ulisababisha pengo la mahitaji ya kufanya ulinganishi baina ya lugha za kundi la JE (Kaskazini) na kundi la G (Kusini) ili kubaini uwiano na tofauti kwa ajili ya ujifunzaji hasa baina ya Luganda na Kiswahili sanifu. Lugha hizi ni lugha ambazo zina ukuruba na zinazotumika katika mazingira ya kijiografia, tofauti moja ikiwa lingua franka na nyingine lugha asili ya Kijamii na ambazo zote zinafundishwa na kutumika nchini Uganda.

Nyanda (2015) akichunguza mwingiliano wa lugha, alitambua kuwa mwingiliano wa lugha mbili tofauti husababisha mwathiriana wa lugha kutokana na kuwa kila lugha kuchukua baadhi ya msamiati na kanuni kutoka lugha nyingine na kuuingiza katika lugha yake. Utafiti wa Nyanda (keshatajwa) ulichochea kufanyika kwa utafiti wa kuchanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Uchanganuzi huu ulikuwa msingi wa kutathimini mwingiliano baina ya lugha mbili tofauti katika viwango vya kiisimu vya mofolojia na sintaksia kutokana na ukaribu baina ya wanajamii wa Luganda na lugha husika ya Kiswahili sanifu katika matumizi. Aidha, uchanganuzi wa kanuni ulisaidi kutathimini jinsi kanuni za Luganda na Kiswahili huingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu katika vipashio vya kisarufi vya nomino (ngeli), viwakilishi nafsi, vikanushi, na vivumishi.

Philipo (2017) akifafanua tofauti baina ya vivumishi na vibainishi katika Lugha ya Kiswahili, alitambua kuwa vibainishi ambavyo kwa mujibu wa maelezo yake ni viwakilishi vya vivumishi hutumika kwa kuzingatia kanuni maalum ya mpangilio wa maneno katika tungo kukumusha nomino. Anaeleza kuwa,

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

huwezi ukawa na kibainishi kinachofuata kibainishi kingine bila kufuata kanuni maalum. Mathalani, wataalamu Rugemarila (2007), Mwihaki (2007), na Lusekelo (2009) wanafafanua kuwepo kwa kanuni maalumu ya mpangilio wa vibainishi katika lugha za Kibantu hususani Kiswahili katika tungo huanza na vibainishi vimilikishi na kufuatiwa na vibainishi vionyeshi.

Kitsao (2015) akichunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi, alitambua kuwa makosa ya kisarufi katika kipengele cha mofosintaksia ulitokana na ukiukaji wa mfuatano wa matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia katika tungo. Aidha, alieleza kuwa tofauti za kimuundo za vipashio vya L1 huathiri matumizi ya vipashio vya kimofosintaksia katika L2. Massamba na wenzie (1999) wakishughulikia viambajengo vya sentensi, walibaini kuwa lugha za Kibantu hushabihiana kimuundo na kisifa. Katika kueleza uwiano wa kanuni ya uambishaji, wanaeleza kuwa lugha za Kibantu huwa na mfuatano wa viambishi ambavyo huambikwa kabla ya mizizi kuwakilisha sifa za kisarufi.

Jerro (2018), katika uchunguzi linganishi wa vipashio vya kimofolojia na kifonolojia vya Kiswahili na lugha zingine tano za Kibantu ikiwemo Luganda, Kinyarwanda, Gikuyu, Kihaya na Proto- Bantu, alitambua kuwa Kiswahili hudhihirisha tofauti za kiisimu ikilinganishwa na lugha nasaba kinyume na matarajio kuwa lugha zilizo na makutano na mtagusano huathiriana na kusababisha mabadiliko. Mathalani, Abdallah (2018) akichunguza uwiano na utofauti wa kiisimu kati ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi, aligundua kuwa kifonolojia lugha hizi mbili hutofautiana kifonimu na katika baadhi ya kanuni za fonolojia na mofolojia hasa katika matumizi ya vipashio vya kisarufi vya nomino, vitenzi na vivumishi vimilikishi.

Mulei (2014) akichunguza athari za Kigisu katika mazungumzo kwa Kiswahili, alitambua kuwepo kwa athari za Kigisu uliojitokeza katika uhamishaji wa kanuni za ukanushaji kutoka L1 hadi L2. Utafiti wake ulipendekeza kufanyika kwa utafiti kuhusu lugha zingine za Kibantu katika jamii za Uganda ili kuchanganua athari zinazojitokeza katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Utafiti wa Mulei (keshatajwa), ulichangia katika kuchanganua kanuni za kimofosintaksia za Luganda katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama msingi wa kutathimini kanuni za kimofosintaksia za Luganda na jinsi zinavyoingiliana na kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu. Aidha, utafiti huu ulichukulia kuwa mfanano na tofauti za kanuni za L1 huweza kusababisha mwingiliano wa mofosintaksia katika matumizi ya L2. Kwa hivyo Makala haya ni matokeo ya utafiti uliochanganua kanuni zinazofafanua mifanyiko ya kimofosintaksia ya Luganda na Kiswahili sanifu katika matumizi, ili kutathimini mwingiliano wa mofosintaksia ya Luganda na jinsi inavyoathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

Onyango (2018) alitambua kuwa ujifunzaji lugha ni tukio la kiutambuzi la mtu kufahamu au kutambua kuwa anajifunza lugha kwa kuzingatia kanuni na muundo wa lugha. Matokeo ya Onyango (ameshatajwa) yanatiliwa mkazo juu ya lengo kuu la taaluma ya isimu ambalo linahusiana na uwekaji wazi kanuni zinazotawala lugha ambazo wazungumzaji wanazitumia bila wao wenyewe kujua. Vilevile, katika kuweka kanuni hizi, Besha (1994) anasisitiza kuwa jambo la msingi na awali ya yote ni kuwa lazima isimu iendeleze namna gani lugha inavyotumika katika jamii bali sio jinsi ya kuzungumza lugha husika. Besha na Onyango (wametajwa) wanaamini juu ya udhihirishaji wazi wa isimu unaotegemea matokeo ya utafiti juu ya matumizi ya lugha katika jamii kuhifadhi kanuni hizo.

Kulingana na Hyman na Katamba (2001); Katamba, F., na Stonham, J. (2006). na Lewis (2009) Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha mbili tofauti zenye mifumo ya kipekee ya kiisimu ya fonolojia, mofolojia na sintaksia zinazotofautiana hata ingawa zote ni lugha za Kibantu. Upekee wa lugha hizi ndio unaozitambulisha na kuzitofautisha

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

lugha hizi kiisimu hasa katika matumizi ya vipashio na kanuni za kiisimu. Aidha, ulinganishi wa mofolojia na sintaksia baina ya lugha 19 za Kibantu za Afrika Mashariki kukiwemo Luganda na Kiswahili, zilidhihirisha kwamba kwa upande mmoja lugha hizi zinafanana kisarufi, lakini kwa upande mwingine zinatofautiana kwa kiasi kikubwa.

Mapitio haya ya maandishi yamebainisha kuwa ingawa kuna tafiti ambazo zimefanyika kuhusiana na kanuni za mifanyiko ya vipashio vya kimofosintaksia za lugha za Kibantu, Kiswahili na Luganda zikiwemo, hakuna utafiti uliofanywa kuchanganua na kudhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za mifayiko ya vivumishi vya Luganda a Kiswahili sanifu. Makala haya ni matokeo ya utafiti wa maktabani unaoripoti kufanana na kutofautiana kwa kanuni za mifanyiko ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili wenye azma ya kukuza na kuendeleza matumizi sahihi ya lugha za Kibantu. Iadha ufahamu wa uwaino na tofauti unatarajiwa kuzuia athari za mwingiliano wa lugha asili katika matumizi ya Kiswahili sanifu.

## NADHARIA YA UTAFITI

Makala haya yaliongozwa na mihimili ya sarufi bia na upatanifu ya nadharia ya Umilikifu na Uhusisho (Chomsky, 1981). Mhimili wa kwanza wa sarufi bia huchukulia kuwa kanuni zilezile za kisintaksia hutumika katika lugha zote, ingawa zinaweza kutofautiana kidogo katika lugha mbalimbali kwa msingi wa data ya lugha hizo. Mhimili wa pili ni wa upatanifu unaofafanua uhusiano wa kimiundo kwa kubainisha sheria ambazo huunganisha vipashio vya sehemu ya sentensi na miktadha ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Mathalani uchaguzi wa nadharia hii ulitokana na madai ya Mulei na wenzie (2021) wanaoeleza kuwa maarifa ya kisintaksia ya mtu yanaweza kuonyeshwa kupitia njia mbili rasmi za kanuni za kimsingi ambazo hupatikana katika lugha zote (ubia wa kanuni za kisarufi) na tofauti za kimofosintaksia za kanuni miongoni mwa lugha huweza kusababisha mwingiliano wa lugha. Nadharia hii iliuongoza utafiti katika kuchunguza sifa za vivumishi kimiundo na kikanuni katika matumizi, kutathimini na kudhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili.

## MBINU ZA UTAFITI

Data ilikusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini kutumia kifaa cha kudondoa data cha orodhahakiki chenye sifa za kimofosintaksia zinazotambulisha kanuni za matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Data za madhumuni hii zilitokana na usomaji na uchanganuzi wa vitabu vya kiisimu vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu kufundishia sarufi na vitabu vya ziada vya kufundishia sarufi ya Luganda na Kiswahili sanifu, tasnifu, majarida, upekuzi wa maandishi na tafiti mbalimbali zilizoandikwa kuhusiana na kanuni za matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu maktabani na mtandaoni. Kwa kutuma mbinu ya usampulishaji dhamirifu kufikia kiwango kinachotosheleza mahitaji ya utafiti ambapo hakuna swala lingine jipya linalojitokeza, jumla ya vitabu na matini 34 viliteuliwa kidhamirifu kusaidia katika uchunguzi wa kanuni za vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Vitabu na matini kumi na sita (16) ya Luganda na kumi na nane (18) ya Kiswahili vyenye kueleza na kufafanua vipashio vya kimofosintaksia vya Luganda na Kiswahili sanifu viliteuliwa kutumika katika utafiti huu.

Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kutumia mbinu ya kimaelezo iliyotumika kutoa picha na msingi wa kufafanua uwiano na tofauti za kanuni za matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Data iliwasilishwa kutumia michoro matawi na maelezo ya moja kwa moja pamoja na nukuu ya kanuni kama inavyofafanuliwa katika maandishi kudhihirisha jinsi kanuni za mifanyiko ya kimofosintaksia ya vivumishi vya Luganda huwiana na kutofautiana na ile ya Kiswahili sanifu. Data iliyohitajika katika utafiti huu ni ile ya uwiano na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

tofauti za kanuni za mifanyiko ya matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Uhakiki Linganishi wa Kanuni za Mifanyiko ya Vivumishi vya Luganda na Kiswahili Sanifu

Matokeo ya uchanganuzi matini kutumia kifaa cha kudondoa data kutoka kwa vitabu teule vya kisarufi vya Luganda na Kiswahili sanifu ulibaini kuwa, licha ya kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha za nasaba moja, kanuni za matumizi ya aina mbalimbali ya vivumishi ulidhihirisha kuwiana na kutofautiana. Uwiano na tofauti hizi zilidhihirisha kuwa lugha hizi ni lugha mbili tofauti zenye aina, maumbo, na miundo ya kipekee ya vivumishi ambayo matumizi yake katika tungo ni ya kipekee kiisimu. Mathalani, kwa kurejelea mihimili ya sarufi bia, data iliyopatikana ilibainisha kuwa kanuni zilezile za kimofosintaksia za matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu zilitumika katika lugha hizi mbili. Hata hivyo, kulitokea tofauti ya kimuundo, na maumbo ya vivumishi, mpangilio, dhima, mahali pa utokeaji, mahusiano ya vivumishi, na maneno makuu katika tungo na urejeleo wa vivumishi. Tofauti hizi zilidhihirisha kuwepo kwa uwiano na tofauti katika kanuni za matumizi ya aina mbalimbali ya vivumishi kuonyesha uhusiano milikifu na Unganifu baina ya aina mbalimbali ya vivumishi na maneno mengine katika tungo kama inavyojadiliwa vifuatavyo:

## UCHANGANUZI LINGANISHI WA KANUNI ZA MIFANYIKO YA VIVUMISHI VYA LUGANDA NA KISWAHILI SANIFU

Kanuni za kimofosintaksia huchunguza utaratibu au sheria za matumizi ya kipashio cha kisarufi kuegemea muundo wake kimofolojia na kisintaksia. Utafiti huu ulichunguza sheria za kimuundo za matumizi ya aina mbalimbali ya vivumishi kimofolojia na kisintaksia kuzingatia nadharia za Umilikifu na Unganifu ya Chomsky (1981). Uchunguza wa kanuni ulizingatia ***uhusiano wa kimiundo*** **kwa kubainisha kanuni ambazo huunganisha matumizi ya vivumishi na maneno mengine katika utungo, na miktadha ya kimiundo ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika.** Matokeo ya utafiti yalidhihirisha uwiano na tofauti za kanuni za kimofosintaksia za matumizi ya vivumishi vya sifa, idadi isiyo kamili, -a Unganifu na vionyeshi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Ufuatao ni uchanganuzi linganishi wa kanuni za kimofosintaksia za matumizi ya vivumishi katika Luganda na Kiswahili sanifu.

### Kanuni ya Muungano na Utawala wa Vivumishi

Matokeo ya uhakiki wa maandishi ya Chesswas (1967); Radford (1997); Mgullu, (1999); Katamba, (2003); Chepkwony (2012) yalibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha ambazo hushabihiana katika matumizi ya kanuni hii ya muungano na utawala wa vivumishi ambayo hushikilia kuwa: Vivumishi huunganika na maneno mengine kuunda virai na uvumishaji hujitokeza katika virai kutokana na nomino kama neno kuu. Pia, kanuni hii inashikilia kuwa neno kuu ndilo linalotawala matumizi ya kivumishi katika kundi nomino ambapo nomino ni kitawala na kivumishi ni kitawaliwa (Radford 1997; Habwe na Karanja, 2004; Egara, 2016) kama inavyodhihirika katika mifano ya Data na (1)

| | |
|---|---|
| *a) Omwana **mumbi** ayimba bulungi nyoo.* | *Mtoto **mfupi** anayimba vizuri sana.* |
| *Abaana **bambi** bayimba bulungi nyoo* | *Watoto **wafupi** wanaimba vizuri sana* |
| *b) Muyizi **wange** anasoma bulungi.* | *Mwanafunzi **wangu** atasoma vizuri* |

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

| | |
|---|---|
| *Abayizi* ***baaffe*** *basoma bulungi.* | *Wanafunzi* ***wetu*** *watasoma vizuri* |
| *c) Omulimi* ***ono/ oyo/ oli*** *omugezi omuneneo* | *Mkulimao* ***huyu/huyo/yule*** *mwerevu mnene* |
| *Abaana* ***aba/abo/bali/*** *batawanya nyoo.* | *Watoto* ***hawa/hao/wale*** *wanasumbua* |
| *d)* ***Ono*** *omwana* ***mulungi*** | ***Huyu*** *mtoto* ***mzuri*** |
| ***Bano*** *abaana* ***balungi*** | ***Hawa*** *watoto* ***wazuri*** |
| ***e) Omw****ana* ***omu****lungi* ***a****manyi okusoma* | ***M****toto* ***m****zuri* ***a****najua kusoma* |
| ***Omw****ana* ***omugezi a****yiise ebigezo* | ***Mtoto mwerevu a****mepita mitihani* |
| ***f)*** *Maama yafumbye emmerre* ***entono.*** | *Mama alipika chakula* ***kichache/kidogo.*** |
| ***Abazimbi*** *banenne* ***balala*** *bazimba.* | ***Wajenzi*** *wanene* ***wengine*** *wanajenga* |

**Data kutokana na ufafanuzi wa Kim, B. M., & Lee, H. A. (2019; 1863). na Abudonia (2014)**

Data (1) ilidhihirishwa uwiano wa matumizi ya vivumishi katika tungo za Luganda na Kiswahili sanifu yanayotokana na muundo wa virai ambapo nomino imetawala matumizi ya vivumishi. Data hii inabainisha kuwa matumizi ya vivumishi katika tungo hutokana na kanuni ya kisarufi ya kuunganisha kategoria mbalimbali za maneno kuzingatia muundo virai kuonyesha utawala na umilikifu wa vipashio katika tungo. Kwa kuegemea mihimili ya Ubia na upatanifu ya nadharia ya Umilikifu na Unganifu ya Chomsky (1981), **utafiti huu uligundua kuwa vivumishi vya Luganda na Kiswahili hutokea katika nafasi tofauti ya tungo na kutawaliwa na nomino kama neno kuu katika utungo ambapo nomino hutawala matumizi ya vivumishi na utokeaji wake katika nafasi tofauti ya tungo baina ya Luganda na Kiswahili sanifu.** Hata tofauti inayojitokeza ni kuwa maumbo ya nomino na vivumishi ya Luganda hutofautiana na ya Kiswahili sanifu kuonyesha kuwa Lugha hizi ni lugha mbili tofauti licha ya kuwa na kanuni moja kama inavyodhihirika katika mifano ya vivumishi vilivyokolezwa katika Data na (1).

**Kanuni ya Umiliki wa Vivumishi**

Kanuni hii ya kimofosintaksia inafafanua mifanyiko ya kimofosintaksia inayochochewa na kategoria ya kimofosintaksia ya uambishaji wa viambishi vya ngeli nomino na idadi ya umoja na wingi katika mizizi ya maneno na mpangilio wa maneno katika tungo virai. Kanuni hii inashikilia kuwa: Lazima nomino iakisiwe katika muundo wa kivumishi katika tungo vinginevyo tungo itakayojitokeza haitakuwa sahihi kisarufi (Chomi, 2003). Kanuni hii ilitumika na Oduor (2017) pamoja na Gromova (2008) kueleza kanuni za upatanishi wa nomino na vivumishi. Kulingana na wataalamu hawa, viambishi awali vya nomino na vya vivumishi, kwa kiasi kikubwa huwa havitofautiani kimaumbo bali huwa vinaandamana na viambishi vya umbo nomino.

Uchanganuzi wa matini ulibaini kuwa, **Luganda na Kiswahili sanifu ni lugha ambazo huzingatia uhusiano wa kategoria za maneno kujenga tungo zenye maana.** Upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na vivumishi huzingatia kwamba viambishi mwanzoni mwa vivumishi na vitenzi katika sentensi huathiriwa na viambishi awali vya ngeli nomino ambamo nomino hiyo imeainishwa (Odour, 2017 Kiyinikibi, 2021). Viambishi ngeli na vibainishi ngeli vinavyokaririwa katika nomino ndivyo vilivyokaririwa katika mizizi ya vivumishi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

vinavyoambikwa kama viambishi nomino kudhihirisha upatanishi wa kisarufi kati ya nomino na vivumishi katika tungo za Luganda na Kiswahili sanifu. Data na (2) inadhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni baina ya Luganda na Kiswahili sanifu:

| | |
|---|---|
| *a) [O-mw]-ana [o-mu]-lungi* | *[a-ba]-na [a-ba]-lungi* |
| *[M]-toto [m]-zuri* | *[Wa]-toto wazuri* |
| *b) [E-ki]-tabu [e-ki]-lungi* | *[E-bi]-tabu ekilungi* |
| *[Ki-]-tabu [ki]-zuri* | *[Vi]-tab [vi]-zuri* |
| *c) [Em]-bwa [en]-nungi* | *[Em]-bwa [n]-nungi* |
| *[-] Mbwa [n]-zuri* | *[-] mbwa [n]-zuri* |
| *d) [e-] ttaayi [e- n-] nungi* | *[ e-] ttaayi [e-n-]lungi* |
| *e) [-]Tai [n]-zuri* | *[-]tai [n-]-zuri* |
| *f) [A-ka]-tale [aka]-lungi* | *[O-bu]tale [o-bu]-ungi* |
| *[-]Soko [n]-zuri* | *[Ma]-soko [ma]-zuri* |

**Chanzo: Data kutoka kwa Kiyinikibi, 2021**

Data na (2) inadhihirisha kuwa muundo wa viambishi na vibainishi nomino ngeli vinavyojitokeza kati ya nomino na vivumishi unatokana na uhusiano uliopo kati ya nomino kama neno kuu na kivumishi. Viambishi hivyo vinapatana na hivyo kusababisha upatanishi au uhusiano wa kisarufi wa kimofolojia kati ya nomino na vivumishi. Uhusiano huo wa kiupatanishi unaonyeshwa na viambishi patanishi vya ngeli nomino ambavyo huambatanishwa kwenye vivumishi. Maumbo hayo hubadilika na kuchukua maumbo mbalimbali kutokana na aina ya kivumishi pamoja na mazingira mengine ya utokeaji wa nomino na kivumishi katika utungo.

Kwa kurejelea mihimili ya Ubia na Upatanifu, utafiti uligunduliwa pia kuwa, ingawa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia viambishi patanishi msingi kuonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino na vivumishi, tofauti inajitokeza katika matumizi ya viambishi patanishi vya msingi vinavyotumika katika uambishaji wa mizizi ya nomino na vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Kiswahili kilitumia viambishi awali vya nomino vinavyotokea katika mazingira mbalimbali kama vile vya kimofofonolojia, mofosintaksia, na ngeli nomino zinazodhihirisha idadi ya umoja na wingi. Luganda hutumia viambishi viwili ambavyo ni viambishi awali vya nomino na vibainishi nomino ambapo mazingira ya utokeaji ulitofautiana na wa Kiswahili hasa kifonolojia na kimofolojia na hivyo kuathiri mofosintaksia ya matumizi ya vivumishi kati ya Luganda na Kiswahili sanifu kama inavyojitokeza katika Data ya mchoro na (1) wa uwakilishi wa viambishi patanishi kati ya nomino na vivumishi:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206




**Chanzo: Kutokana na Uchanganuzi wa data ya kanuni ya Umilikifu wa vivumishi.**

**Kanuni ya Kimofolojia ya Uundaji Vivumishi**

Kanuni hii hushikilia kuwa: Vivumishi katika lugha za Kibantu huchukua maumbo mbalimbali. Maumbo hayo ni maumbo yanayoambishwa na maumbo yasiyoambishwa. Vilevile, maumbo ya vivumishi vinavyoambishwa hufuata kanuni ya kimofolojia ya uambishaji inayodai kuwa: Uambishaji maneno kisarufi huzingatia upangaji wa viambishi vyenye sifa za kisarufi (uambishaji kisarufi) na uambishaji kirai unaozingatia upatanishi wa kisarufi wa viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya maneno hutokana na nomino kama neno kuu kama inavyojitokeza katika mifano ya Data na (2). Kimofolojia, data (2) inadhihirisha muundo wa vivumishi kuchukua maumbo sawa ya viambishi ngeli vya nomino kimofolojia kuwakilisha ngeli na idadi ya umoja na wingi na nomino au kirai nomino ambayo inathiri umbo la vivumishi kama ilivyoelezwa na wataalamu Odour (2017); Mgullu (1999); Massamba na wenzake (2012).

Uchanganuzi wa data za maktabani za maandishi ya Katamba, (2003); Chomi (2003); Mgullu (1999); Habwe na Karanja (2004) yalidhihirisha kuwa kimofolojia, vivumishi vya Luganda na Kiswahili huundwa kwa viambishi patanishi pamoja na mzizi wa kivumishi. Kimofosintaksia, muundo wa ngeli nomino uliweza kuathiri maumbo ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili katika kirai nomino hasa kwa kuzingatia mianzo au viambishi awali vya nomino. Maumbo yaliyoanza na konsonanti yalionyesha kutoathiri viambishi vinavyopachikwa mwanzoni mwa mizizi ya vivumishi huku vivumishi vilivyoanza na irabu kuathiri viambishi awali vya vivumishi katika virai. Athari hii ilisababisha mabadiliko ya kimofofonolojia ya aina mbalimbai za vivumishi kuanzia vivumishi sahili na changamano.

Matokeo ya uchanganuzi ilidhihirisha kuwa kanuni ya kimofolojia ya uundaji wa vivumishi ya Luganda na Kiswahili sanifu ilishabihiana hasa katika uambishaji wa viambishi awali kwenye mizizi ya vivumishi kutokana na viambishi ngeli vya ngeli nomino za Luganda na Kiswahili sanifu katika kirai nomino. Hata hivyo, maumbo ya viambishi vya uambishaji yalitofautiana kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Luganda ilitumia maumbo tofauti katika vivumishi kutokana na tofauti ya maumbo ya ngeli kimofolojia. Pia, Luganda ilitumia vibainishi ngeli na viambishi ngeli mwanzoni mwa mizizi ya vivumishi kutegemea nomino kuu katika tungo nomino. Kiswahili iliambisha viambishi awali vya nomino kwa kuzingatia maumbo ya kimofolojia kwenye mizizi ya kivumishi. Aidha, mabadiliko yanayotokea katika viambishi patanishi kati ya Luganda na Kiswahili yalitofautiana kutokana na sifa za kifonolojia, kimofolojia na kifonetiki ya viambishi awali ambavyo viliathiri viambishi vinavyopachikwa mwanzoni mwa nomino na vivumishi katika virai nomino. Kulingana na

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

maelezo haya, viambishi vipatanishi msingi vya vivumishi katika Luganda na Kiswahili sanifu huchukua maumbo tofauti kutokana na aina ya vivumishi pamoja na mazingira inamotokea (Chomi, 2003) kama inavyojitokeza katika mfano wa Data na (2) hapo juu.

Aidha, ilibainika pia kuwa utaratibu wa kuambishi vivumishi katika kirai, vivumishi hufuata nomino kuu. Utaratibu huu hutofautiana kutoka ngeli moja hadi nyingine na aina ya vivumishi vinavyohusika. Kwa mfano katika vivumishi vionyeshi, Kiswahili hutanguliwa na mizizi ikifuatwa na kiambishi cha ngeli katika ujenzi wa vionyeshi tofauti na Luganda inayotanguliwa na kiambishi ngeli ikifuatwa na mzizi wa kionyeshi kama inavyojitokeza katika data ya mchoro na (2) wa Matawi ya darajia za vivumishi vimilikishi:




**Data kutokana na Uchanganuzi wa maandishi ya Katamba (2003) na Mgullu (1999)**

**Kanuni ya Mabadiliko ya Kimofofonolojia ya Uundaji wa Vivumishi**

Kanuni hii inashikilia kuwa: Kuna mabadiliko ya kimofofonolojia yanayotokea katika viambishi patanishi na katika mizizi ambayo inapaswa kuelezwa kudhihirisha muundo wa aina mbalimbali ya vivumishi na athari za matumizi kimazungumzo au kimaandishi kwa mujibu wa lugha mbalimbali. Fonimu zinazoathiri viambishi patanishi na kusababisha mabadiliko ya fonolojia ni irabu na konsonanti. Mfuatano wa irabu au konsonanti katika mazingira ya fonimu fulani huweza kusababisha athari ya viambishi vipatanishi vya nomino na vivumishi katika kirai nomino. Irabu ikifuatwa na irabu, mabadiliko huweza kutokea na kusababisha fonimu nyingine ya kiambishi kipatanishi. Aidha, konsonanti ikifuatwa na konsonanti au irabu, huweza kusababisha mabadiliko ya viambishi vinavyopachikwa kwenye mizizi ya vivumishi (Chomi, 2003 na Massamba na wenzake 2004).

Kwa mujibu wa kanuni hii, kiambishi kipatanishi msingi kikiongezwa kwenye mzizi wa kivumishi kunatokea mabadiliko ya muundo wa kiambishi kipatanishi cha msingi wa mzizi wa kivumishi kinachotumika pamoja na nomino kuu katika tungo. **Luganda na Kiswahili sanifu zilidhihirisha maumbo ya kifonolojia katika matumizi ya fonimu mbalimbali kutegemea aina za vivumishi na ngeli ambamo nomino huanishwa** (Katamba, 2003; Chomi 2003; Habwe na Karanja 2004; Mgullu 1999). Kanuni ilijitokeza na kanuni mbalimbali katika Data na. (3)**:**

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **a** | + | **e** | → | **e** | **wa** | + | **enyewe** | **wenyewe** |
| **i** | + | **e** | → | **y** | **li** | + | **enye** | **Lenye** |
| **u** | + | **e** | → | **w** | | | | |
| **u** | + | **a** | → | **a** | | | | |
| **a** | + | **u** | → | **u** | | | | |
| **i** | + | **a** | → | **a** | | | | |
| **a** | + | **i** | — | **e** | | | | |
| **i** | + | **i** | → | **i** | | **mingi** | | |
| **i** | + | **u** | → | **u** | | | | |
| **a** | + | **o** | → | **o** | | | | |

Data na (3) inadhihirisha baadhi ya kanuni za mabadiliko ya kimofofonolojia ambayo kwayo yanatokana na udondoshaji, uyeyushaji muunganiko na tangamano la fonimu ambayo husababisha mabadiliko ya viambishi vipatanishi msingi vinavyopajika kwenye viambishi vya mzizi wa vivumishi katika tungo viarai. Kanuni hii hujitokeza kutokana na aina mbalimbali ya vivumishi inayotokea katika kundi nomino mbalimbali. Aidha, mabadiliko haya hujitokeza katika vivumishi vionyeshi, visisitizi, vivumishi viulizi, vimilikishi, visifa na vivumishi vinginevyo vinavyoambikwa. Kwa kurejelea mihimili ya Ubia na Upatanishi ya nadharia ya umilikifu na Unganifu, utafiti huu ulitambua kuwa **ingawa mabadiliko ya Kimofofolojia hujitokeza katika Luganda na Kiswahili, mchakato wake hutofautina kutokana na tofauti za kifonimu kati ya Luganda na Kiswahili sanifu**. Hali iliyodhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili ni lugha mbili tofauti zenye kanuni ambazo licha ya kuwa zinafaanna, huweza kutofautiana katika michakato na matumizi ambayo yasiposingatiwa matumizi bora huweza kupotoshwa.

**Kanuni ya sarufi muundo virai**

Kanuni hii huchunguza mpangilio au mfuatano wa kategoria za kisarufi zinazokubalika kuunda sentensi na upambanuzi wa muundo wa ndani wa sentensi. Kanuni hii inadai kuwa upatanifu wa kisarufi katika utungo hutawaliwa na vipashio vya kimofosintaksia na vipashio hivyo huathiriana ambapo kipashio cha kwanza hutegemea sana kipashio cha pili ili kuleta maana. Kanuni hii huchunguza kategoria za maneno na msamiati pamoja na uhusiano unaohusika katika ujenzi wa sentensi.

Uchanganuzi wa data za Habwe na Karanja (2004); Chomi, (2003) na Abudonia (2014) kurejelea mihimili ya Ubia na Upatanishi, **ilibaini kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kanuni ya muundo virai katika maandishi na mazungumzo yao**. Tungo nyingi zilizojitokeza ziliweza kubainishwa kwa kutumia kanuni ya kikategoria na uainishaji wa maneno ya kikategoria. Vivumishi vilidhihirika katika sentensi vikiwa vinatawaliwa na nomino kama neno kuu. Kiutaratibu, vivumishi vilivyotokea baada ya nomino vilichukua aidha nafasi ya pili na tatu au kutokea mwishoni mwa sentensi kutegemea aina ya sentensi (Abudonia,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

2014; Kiyinikibi, 2021; Mbillow, 2017) kama inavyojitokeza katika mifano ya Data na (6):

a) *Omuyizi* ***omulungi*** *asomwe ekitabu* ***bulungi****Mwanafunzi* ***mzuri*** *amesoma kitabu vizuri*

b) *Omuyizi* ***ono*** *asomye ekitabu* ***bulungi*** *Mwanafunzi* ***huyo*** *amesoma kitabu vizuri*

c) *Omuwala* ***oli omunene*** *ayimbye* ***bbubi*** *Mwanafunzi* ***Yule mnene*** *ameimba vibaya.*

**Chanzo: Data kutokana na uchanganuzi wa Abudonia, (2014: 38-41) na Leah na Sseguya (2015: 29-33)**

Data na (6) inabainisha kuwa nomino hufuatwa na kivumishi kimoja, au viwili ambayo hutokea pamoja baada ya nomino. Vivumishi hivi hutokea katika mazingira maalumu ikiwakilishwa na kategoria ya maneno yenye uhusiano. Vivumishi hivi hutokea katika kirai nomino na huathirika na nomino kama neno kuu. Athari hii inatokana na viambishi vinavyopachikwa mwanzoni mwa mizizi ya vivumishi (Abudonia 2014; Mbwillow 2017; Kisakwah 2014; Ferrari-Bridgers 2008; Balagadde 2016; Dixon 2010; Faki Juma 2019).

Tofauti inayojitokeza kuhusiana na utokeaji wa vivumishi katika Luganda na Kiswahil sanifu ni changamani ambapo inahitaji kuelezwa ili kutambua utaratibu na utokeaji wa kanuni hii. Kilichotambulika ni kuwa, vivumishi vya Luganda na Kiswahili hujitokeza katika kirai nomino kutegemea muktadha wa mazungumzo na kanuni za lugha husika. Kwa mujibu wa kanuni hii, dhima ya vihusishi katika KN hufanya kazi kama vivumishi na katika KT hufanya kazi kama vielezi ambapo uhusiano wake hujenga tungo sahihi za lugha ikitumika vikamilifu.

Kanuni ya sarufi muundo virai pia iliweza kujidhihirisha kupitia kwa vishazi. Ilidhihirishwa kuwa vivumishi katika Luganda na Kiswahili sanifu hujitokeza katika vishazi. Vivumishi hujitokeza katika vishazi kama sentensi sahili iliyoshushwa hadhi. Huku, vishazi tegemezi vikifanya kazi kama kivumishi (Mbwillow, 2017; Dixon, 2010). Kwa mfano Data na (7)

a) *Abayimbi abayimbye.*
*Wanamziki ambao wameimba*

b) *Abayizi abasoma.*
*Wwanafunzi ambao wanasoma*

c) *Abaana abazannya Watoto ambao wanacheza*

**Chanzo: Data kutokana na maelezo ya Dixon, (2010) na Mgullu (1999)**

Data na (7) Ilidhihirisha utokeaji na matumizi ya kanuni ambayo hutokana na muundo wa KN kuundwa kwa nomino [N] na kishazi [Kz] kinachofanya kazi kama kivumishi [V]. Kanuni hii vilevile inaweza kuwakilishwa kwa njia mishale Na (8) na ya matawi ya mchoro Na. (3) zifuatazo:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

a) *Njia ya mishale*

KN ⟶ N + V [Kz]

b) *Njia ya matawi Na (3) kuwakilisha kanuni ya utokeaji wa vivumishi katika vishazi*




Kwa kuzingatia mihimili wa Ubia na Upatanishi, Luganda na Kiswahili sanifu zilidhihirisha kutumia kanuni hii katika mazungumzo na maandishi yao kwa kuwakilisha vivumishi katika vishazi ambapo nomino hutangulia kishazi tegemezi kinachofanya kazi kama kivumishi. Tofauti iliyojitokeza ni ya maumbo ya viambishi vinavyopachikwa kwenye vitenzi kuwakilisha urejeshi. Kiswahili hutumia 'amba na o' rejeshi [***ambao*** *na wana****o****soma*] huku Luganda ikiwakilisha utegemezi katika wakati na ambao haudhihirishi viambishi bali uleksika unaojitokeza kidhahania na kimuktadha. Aidha, vivumishi vya Luganda vinaweza kuundwa kutokana na vitenzi kwa kubadilisha kiambishi tamati cha kibantu */-a/* na */-e/* kinyume na Kiswahili sanifu. Vivumishi vya Luganda ni vivumshi ambavyo huwa na uhusiano mkubwa na nomino au kiwakilishi cha nomino. Uhusiano wa kivumishi hiki hudhihirishwa kwa viambishi vya ngeli vinavyowakilisha umoja au wingi. Viambishi hivi huambishwa kwa mzizi wa kivumishi kuonyesha upatanishi wa kisarufi wa nomino au kiwakilishi chake kwa umoja na wingi (Leah na Sseguya, 2014) kama inavyojitokeza katika mifano ya Data na (8):

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| *Omu-ntu* | *omu-* | *dukavu* | *aba-* | *ntu* | *aba-* | *dukavu* |
| *M -tu* | *mw-* | *eusi* | *Wa* | *tu* | *wa-* | *eusi* |

Katika mfano wa Data na (10) kutokana na Leah na Sseguya (2014), kiambishi cha umoja ni (o)mu- na kwa wingi ni (a)ba-. Yafaa ikumbukwe kuwa katika Luganda, viambishi vya ngeli vinavyodhihirisha umoja na wingi hutanguliwa na vibainishi vya ngeli vya a-, o- na e- vikifuatwa na viambishi ngeli ambavyo vyote huwekwa nyuma ya mzizi au shina la nomino au kivumishi chake kuwakilisha umoja na wingi wa nomino inayozungumziwa katika utungo wa sentensi. Aidha, viambishi hivi huenda vikibadilika kulingana na ngeli nomino inayotajwa katika utungo, huku kivumishi kikihifadhi nafasi yake bila kubadilika. Hii ina maana kuwa viambishi vya kivumishi cha nomino 'mtu' ni tofauti na 'gari' kwa mfano; '*Omuntu omudukavu/ Mtu mweusi'* sio sawa na '*emmotoka endukavu/ Gari leusi'* ingawa lugha zote zina mzizi {*-dukavu/ -eusi*} ya vivumishi ambavyo huambishwa viambishi nomino.

### Kanuni ya Utokeaji wa Kivumishi Karibu na Neno Kuu

Kanuni hii hutumika kubainisha elementi muhimu katika tungo. Kanuni hii ilitumika na Lusekelo (2017) kubainisha elementi muhimu kati ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

vionyeshi na vivumishi katika KN. Kanuni hii iliasisiwa na Rijkhoff (1986). Kanuni hii inashikilia kuwa nomino kuu au neno kuu katika utungo huwakilishwa au huzingirwa na vibainishi au kirejeleo nomino (kiambishi nomino), kivumishi cha nomino na uhusika milikishi (Kivumishi na uhusika wa nomino). Kanuni hii huamini pia kuwa: neno kuu katika utungo huchagua kuathiri maneno mengine kutegemea mazingira ambamo nomino tajwa hutokea. Kulingana na kanuni hii, nomino kama neno kuu hutawala maneno mengine katika tungo virai na maneno hayo hutokea kwa karibu sana na nomino kuu au neno kuu katika tungo. Kwa mjibu wa Rijkhoff (1986), Vivumishi (vimilikishi na vionyeshi) huchukua nafasi karibu na nomino kama neno kuu katika tungo virai hasa katika Lugha za Kibantu.

Data za maktabani zilidhihirisha kuwa, Luganda na Kiswahili sanifu hudhihirisha matumizi ya kanuni ya ukaribu wa neno kuu na maneno mengine katika tungo virai hasa katika matumizi ya nomino kama neno kuu na vivumishi katika tungo virai kama ilivyoelezwa na Ndomba, 2006; Rugemalira, 2007; Iori, 2015). Matumizi haya ni yale yanayonyesha uhusiano milikifu na unganifu wa nomino kama neno kuu na maneno mengine katika tungo kama inavyojitokeza katika mifano ya Data na (9):

a) *Omuyizi* **omuwamvu** azanye *omupiira* **ggwe** bulungi

N V T N V E

b) *Mchezaji* **mrefu** amecheza *mchezo* **wake** vizuri

N V T N V E

c) *Omulezi* **oyo** adduka

N V T

d) *Mvulana* **huyo** anakimbia

N V T

**Chanzo: Lusekelo, (2017)**

Data katika Mifano Na (9) ya vishazi hivi katika Luganda na Kiswahili sanifu vinadhihirisha matumizi ya vivumishi vimilikishi, vionyeshi na vivumishi vya kimo au sifa kudhihirisha kuwa vivumishi hutokea karibu sana na nomino katika virai nomino (KN) na virai tenzi (KT). Maneno yaliyowekwa katika italiki ni nomino na yaliyokolezwa ni vivumishi ambavyo vimetoka baada ya kutajwa kwa nomino (N). Kwa kutumia njia ya matawi, sentensi ya kwanza inadhihirisha nafasi ya utokeaji wa nomino (N) na neno kuu katika virai husika kama inavyojitokeza katika Mfano wa data katika mchoro Na (4):

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

*Mchoro unaowakilishi kanuni kimchoroti*




*Tanbihi: Kundi nomimo ya kwanza (KN1) na kundi nomino ya pili (KN2)*

Kwa mujibu wa mchoro wa mfano wa Data na(4) matawi haya imedhihirishwa kuwa kivumishi kimetokea karibu na neno kuu ambalo ni nomino [**Omuyizi/mwanafunzi**] katika kirai nomino. Kishazi hiki kimeundwa kwa vishazi viwili, moja ikiwa inetokea katika KN1 na ya pili ikiwa imetokea kulia chini ya KT. Hata hivyo kwa mujibu wa kanuni ya matumzi ya vivumishi, vivumishi hutokea sana katika Kn kuelezea zaidi juu ya nomino kama neno kuu katika utungo. Aidha, vivumishi vilivyokolezwa vimetokea baada ya neno kuu katika KN. Matumizi haya yanadhihirisha kuwepo kwa ubia na upatanishi wa kisarufi wa nadharia ya umilikifu na Unganifu. Luganda na Kiswahili sanifu zinadhihirsha unasaba katika matumizi ya kanuni hii. Hata hivyo tofauti zinajitokeza katika dhima na maumbo ya nomino na vivumishi licha ya kuwa vinatokea katika nafasi moja. Hali hii inaonyesha kuwa ugha hizi ni lugha mbili tofauti na kuhamisha kanuni au maumbo ya matumizi ya vivumishi katika tungo kuwakilisha uhusiano milikifu na unganifu huweza kuathiri matumizi ya Kiswahili sanifu.

**Kanuni ya Uwakilishaji Dhima wa Matumizi ya Nomino Katika Tungo**

Luganda na Kiswahili sanifu hutumia kanuni ya uwakilishi dhima ya viambishi vinavyopachikwa kwenye nomino na mizizi kuwakilisha upatanisho wa kisarufi kati ya nomino na kivumishi katika kirai nomino. Viambishi na mashina yote yanayopachikwa kwenye kategoria ya maneno ya kisarufi lazima iwakilishe dhima ya kimofosintaksia kiuamilifu na kimuktadha. Kwa mujibu wa uchanganuzi wa matini kutumia kifaa cha kudondoa data, maandishi ya Abudonia (2014), Baertlein na Sseguya (2014), Massamba na wenzake (2007) na Philipo, (2017), kuhusu kanuni hii, ilibainika kuwa mizizi ya vivumishi hubeba maana ya kileksika ya vivumishi hivi. Mizizi hii huambishwa kwa namna tofauti kutegemea nomino inavyovumishwa na viambishi hivyo hutumika kuwakilisha neno kuu katika tungo, uwakilishi wa jinsia ya kisarufi, ngeli na idadi ya umoja na wingi pamoja na upatanishi wa nomino na kivumishi katika neno kuu. Dhima ya kivumishi hutokana na kanuni ya uanishaji wa vivumishi husika ambavyo vimesitiriwa katika shina au mzizi wa kivumishi chenyewe kama inavyojitokeza katika mifano ya Data na (10)**:**

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

| | |
|---|---|
| *a)* ***Omu****zannyo* ***gu-****no* ***omu-****lungi* ***gu****sanyibwa.* | ***M****chezo hu****u*** ***m-****zuri* ***u****nachezwa.* |
| ***E-mi-****zannyo* ***gi****no* ***e-mi-****lungi* ***gu****sanyibwa.* | ***Mi-****chezo h****i-i*** ***mi-****zuri* ***i****nachezwa.* |
| *b)* ***E-ki-****tabu* ***Ki-****no* ***e-ki-****lungi* ***ki****guume.* . | ***Ki****tabu hi****ki*** ***ki****zuri* ***ki****tunze.* |
| ***Ebi****tabu* ***bi****no* ***ebi****lungi* ***bi****guume.* | ***vi****tabu hi****vi*** ***vi****zuri* ***vi****tunze.* |
| ***c)*** ***Omu****zzadde* ***w****ange* ***omu****lungi ayimba.* | ***M****zazi yangu* ***m****zuri* ***a****naimba.* |
| ***Aba****zzadde* ***b****ange* ***aba****lungi baimba.* | ***wa****zazi* ***w****angu* ***wa****zuri* ***wa****naimba.* |

***Chanzo:*** **Baertlein na Sseguya, (2014)**

Kwa mujibu wa mifano katika Data na (10) Fonimu na mofimu zilizokolezwa zimetumika katika tungo kuwakilisha viambishi awali vya nomino pamoja na vibainishi vya nomino. Viambishi hivi hutumika kuwakilisha idadi ya umoja na wingi, uainishaji wa nomino na kivumishi ambamo nomino na kivumsihi hutokea au humilikiwa na uhusiano wa kisabaki kati ya nomino na vivumishi katika tungo nomino. Dhima ya upatanisho wa kisarufi umetokana na viambishi vinavyofanana kati ya nomino na vivumishi katika Kiswahili sanifu na vibainishi na viambishi ngeli nomino katika Luganda kama unavyojitokeza katika data ya mchoro Na (5) wa matawi wakilishi ya kanuni.

*Mchoro Na (5): Matawi yanayodhihirisha ya kanuni ya uwakilishaji dhima*




Mchoro Na (5) unadhihirisha dhima ya kila kiambishi na mzizi (Mz) katika utungo kati ya Luganda na Kiswahili sanifu. Kwa kurejelea mihimili ya ubia na uptanishi, imebainika kuwa viambishi vya nomino na vivumishi katika Luganda na Kiswahili vinafanana. Tofauti ni kuwa Kiswahili hutumia viambishi awali vya ngeli nomino ambamo nomino imeainishwa, huku Luganda ikitumia viambishi viwili; kibainishi [Kb] na Kiambishi ngeli [K]. Tofauti nyingine inayojitokeza ni utaratibu wa kuambisha vivumishi vionyeshi kati ya Luganda na Kiswahili sanifu ambapo katika Luganda utaratibu wa uambishaji ni wa kiambishi awali cha ngeli na mzizi huku Kiswahili sanifu kikiambisha dhima ambapo mzizi huja baada ya kiambishi awali. [kihi] ambacho kinaandikwa na kutamkwa kama [hiki].

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

**Kanuni ya Darajia ya Utokeaji wa Vivumishi Katika Tungo Virai**

Kwa mujibu wa kanuni hii, mpangilio au utokeaji wa vivumishi pamoja na neno kuu katika tungo huzingatia utaratibu maalumu katika sentensi. Vivumishi katika tungo hutokea baada ya Nomino (neno kuu) kwa kufuata utaratibu wa vibainishi au viambishi ngeli vya nomino kuu [KB], nomino [N]-Vivumishi [V] na kishazi rejeshi [KZR], kwa muhutasari kanuni ya kidarajia ya matumizi ya vivumishi inaweza kuwakilishwa kama [KB-N-V-KZR]. Aidha, kanuni hii ilidhihirisha kuwa vivumishi vinaweza kutumika kwa pamoja na viambishi ngeli au vibainishi vya nomino na viambishi vimilikishi au viambishi vya uhusika milikishi ambavyo hutokea karibu na neno kuu au nomino kama neno kuu. Kanuni hii inarejelea kanuni ya uambishaji wa viambishi katika vivumishi kutegemea viambishi ngeli vya nomino kama neno kuu inayodai kuwa: Vibainishi na viambishi ngeli vyote vinavyotumiwa katika umbo nomino hutawala viambishi vyote vinavyotumiwa katika maneno ya kategoria ya kisarufi kimofolojia katika tungo kama viwakilishi jirejee.

Kwa mujibu wa kanuni hii; ilidhihirishwa kuwa Luganda na Kiswahili sanifu zilitumia vibainishi na viambishi ngeli katika nomino na vivumishi kwa kutumia utaratibu wa utokeaji wa vivumishi karibu na nomino kuu katika tungo. Mkabala huu ulijitokeza katika uambishaji ambapo viambishi vya nomino viliwekwa mwanzoni mwa vivumishi karibu na nomino kuu hasa vikiambishwa kwenye mizizi ya vivumishi vilivyotumika. Kwa ajili ya utaratibu huo, kulitokea mfanano wa viambishi ngeli na vibainishi nomino katika matumizi ya nomino na vitenzi katika utungo (Massamba, 2004, Lusekelo, 2017). Mfanano huo wa viambishi awali vya nomino na vivumishi ndivyo vilivyobeba dhima ya upatanishi wa kisarufi kati ya nomino kama neno kuu na kivumishi kilichotumika katika tungo kidarajia na kiutokeaji. Pia, kwa kuzingatia utaratibu wa uambishaji, maumbo yanayopachikwa kwenye vivumishi hubadilika kutegemea nomino ambamo nomino husika huainishwa (Chomi, 2003). Viambishi hivi vilitokea mwanzoni mwa vuvumishi karibu na baada ya nomino kuu husika katika utungo kama inavyojitokeza katika mfano wa Data na (11):

| | Luganda | Kiswahili sanifu |
|---|---|---|
| a) | ***A-ka***-*tale* ***a-ka***-*lungi* | ***M***-*toto* ***m***-*zuri* |
| b) | ***E-n***-*nyumba* ***e-n***-*nene* | ***Mi***-*kate* ***mi***-*nene* |
| c) | ***E-ki***-*tanda* ***e-ki***-*nene* | *K**i***-*tanda* ***ki***-*kubwa* |

***Chanzo***: *Uchanganuzi wa data kutokana na Baertlein na Sseguya, (2014)*

Aidha, kwa kuzingatia mihimili ya ubia na upatanifu wa utaratibu wa mpangilio wa maneno katika tungo, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili huzingatia utaratibu wa kivumishi kufuata nomino kuu katika kundi nomino (KN). Hata hivyo, utokeaji wake hutawaliwa na kanuni ya kipragmatiki ya kubainisha kategoria ya kivumishi kipi kifuate kipi kulingana na hadhi (ukuu wa kivumishi) ya kivumishi husika katika kundi nomino (KN). Kanuni hii ilidhibitika kutokana na utafiti wa awali wa Abudonia (2014). Tofauti inayojitokeza katika matumizi ya vivumishi ni ya kipragmatiki ambapo Luganda mara nyingi huweza hata kubadilisha muundo wa kivumishi kutangulia nomino kutegema muktadha na umilisi wa lugha. Kwa mjibu wa utafiti huu, dhima kuu katika Luganda ni kuwasiliana pasi kujali baadhi ya kanuni za kisarufi kama inavyojitokeza katika m**fano wa data katika mchoro Na (6) wa Uwakilishaji wa nafasi ya utokeaji wa vivumishi katika KN**

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206




Data hii inadhihirisha darajia ya matumizi ya vivumishi katika tungo virai ambapo nomino ndilo neno kuu. Kulingana na utaratibu huu, viambishi vinavyokaririwa mwanzoni mwa neno kuu ndivyo vinavyokaririwa mwanzoni mwa vivumishi na hutokea karibu na baada ya nomino. Aidha, katika utafiti huu ilitambulika kuwa nafasi ya utokeaji wa viambishi katika vivumishi vilivyo karibu na neno kuu pia hutegemea uainishaji wa neno kuu katika tungo, aina ya kivumishi na ngeli na idadi ambamo nomino husika hutokea. Vibainishi na viambishi ngeli vilivyokolezwa vinadhihirisha utokeaji huo.

Tofauti iliyojitokeza ni kuwa Luganda ilitumia vibainishi nomino na viambishi nomino awali katika kuambisha vivumishi katika nafasi sawa ya utokeaji (baada ya nomino) wa vivumishi pamoja na nomino kuu katika tungo virai. Vivumishi hivi vilifuata utaratibu wa kutokea baada ya nomino kuu.

Hata hivyo, baadhi ya vivumishi huchukua mkondo tofauti hasa matumzi ya kiambishi huru cha kutaja ujumla wa nomino. Miongoni mwa kivumishi hiki ni [Buli] ambacho kwa kuzingatia utaratibu huu hutokea kabla ya nomino na hakitumii uambishaji wa viambishi nomino wala vibainishi vya nomino. Kiswahili kiliweza kutumia viambishi nomino kimofolojia kuwakilisha au kuonyesha upatanishi wa kisarufi kati ya nomino kuu na vivumishi mbalimbali ambavyo vilijitokeza kulingana na muktadha wa mawasiliano. Viambishi awali vya nomino vya ngeli za Kiswahili kimofolojia vilivyokaririwa katika nomino kuu ndivyo vilivyopachikwa kwenye mizizi ya vivumishi mwanzoni baada ya nomino kuu kutegemea mazingira mbalimbali na uainishaji ambamo nomino husika hutokea kama inavyojitokeza katika mfano wa Data na (12):

a) ***Omusomesa omunene*** *yakubye* ***buli*** *muntu.*

b) ***Mwalimu mnene*** *alipiga* ***kila*** *mtu*

c) ***Omubak****a* ***omulungi*** *yagabira ebilabo buli omuntu yakiliza*

d) ***Mbunge mwem****a hutoa zawadi kwa* ***kila*** *mtu aliyekubali*

Chanzo: Uchanganuzi wa data kutokana na Baertlein na Sseguya, (2014), Luganda (n.d)

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

Data (12) inadhihirisha matumizi ya kivumishi cha jumla katika Luganda *[buli]* ambacho kwa kuzingatia kanuni ya darajia ya ukuu wa matumizi ya vivumishi, ilidondosha vibainishi na viambishi ngeli na ikawa inatokea nyuma ya nomino badala ya kutokea baada ya nomino kama neno kuu. Matumizi haya kwa mjibu wa mjadala wa walimu na wanafunzi ni kuwa haibadiliki kimatumizi na huwa haizingatii uambishaji wa viambishi awali vya nomino na vibainishi ngeli.

Kiutaratibu, ilidhihirishwa kuwa vivumishi mbalimbali vya Luganda na Kiswahili viliweza kutokea kwa pamoja katika utungo. Utaratibu wa matumizi ya vivumishi hivi katika tungo virai ilidhihirisha utata kimatumizi. Luganda na Kiswahili sanifu ilionekana kutanguliza kivumishi kionyeshi (kio) au wakati mwingine kutanguliza kivumishi kimilikishi katika tungo. Katika Uchanganuzi, ilidhihirika kuwa Luganda na Kiswahili hutumia vivumishi kwa njia ya mpishano wa nafasi hasa wakati wa kutumia vimilikishi na vionyeshi. Hata ingawa tafiti za hapo awali zinaeleza kuwa kivumishi kionyeshi huja baada ya neno kuu na hutangulia vivumishi vingine katika tungo (Iori, 2015). Kanuni hii ya matumizi ya vivumishi ilitokana na dhana kuwa ujumbe muhimu katika tungo hutokea kushoto mwa tungo virai hasa katika lugha zinazofuata utaratibu wa kuanza na kiima, kitenzi na kumaliza na yambwa. Aidha, lugha nyingi za Kibantu hukubali vionyeshi kutokea katika nafasi ya viwakilishi nomino au kufuata neno kuu katika kirai nomino (Van de Velde, 2005 na Rizzi, 1997). Hali hii ilitetewa na Chipeta (2016) na Koech, (2013) walinashikilia kuwa utaratibu wa matumizi ya vivumishi katika tungo virai hufuata utaratibu wa nomino kama neno kuu kutangulia, kimilikishi kufuata neno kuu na mwisho kionyeshi.

Utafiti huu ulitambua kuwa Luganda na Kiswahili sanifu hutumia vivumishi katika kirai nomino ambapo kirai nomino huja mwanzo na kufuatwa na vivumishi. Matumizi ya kivumishi kipi hutangulia baada ya nomino kama neno kuu katika kirai hutegemea muktadha wa mawasiliano na dhima ya mawasiliano ya mzungumzaji au mwandishi. Aidha, ilibainika kuwa Luganda na Kiswahili huweza kuambatanisha au kuunganisha vivumishi na nomino (NV) au viwakilishi nomino katika matumizi yake kama inavyojitokeza katika mfano wa data (13)

| | | |
|---|---|---|
| *[Mamawe] wuyo atuuze* | *[Mamake] ndiye yule amefika* | *mama yake ndiyo yule amefika* |
| *[Kitawe] ono alimba* | *[babake] huyu anadanganya* | *baba yake huyu anadanganya* |
| *NV Kio T* | *NV Kio T* | *N V Kio T* |

**Tanbihi: Nomino (mama) na Kivumishi (ya(*ke*)) Kionyeshi (Kio) Kitenzi (T)**

## HITIMISHO

Kwa kuhitimisha, utafiti huu huu ulidhihirisha uwiano na tofauti za matumizi ya kanuni za kimofosintaksia za vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Kufanana na kutofautiana kulijitoze katika matumizi ya kanuni za kimofosintaksia za vivumishi vya sifa, idadi isiyo kamili, -a Unganifu na vionyeshi vya Luganda Katika Kiswahili sanifu. Ilibainika kuwa licha ya kuwa lugha hizi ni lugha za nasaba moja zenye uwiano wa matumizi ya kanuni za kimofosintaksia za vivumishi katika tungo kuonyesha uhusiano milikifu na Unganifu, kuna tofauti ambazo zinajitokeza katika matumizi ya kanuni hizi kimuundo, kiutaratibu, kimuktadha, kimaumbo na aina ya kivumishi kinachohuska katika matumizi ya kanuni ambamo uhusiano huo wa kiunganifu hutumika. Uwiano na toauti hizi zilidhihirisha kuwa Luganda na Kiswahili licha ya kuwa lugha za nasaba moja, ni lugha mbili tofauti kiisimu.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

**Mapendekezo**

Utafiti huu ulichunguza kufanana na kutofautana kwa kanuni za mofosintaksia za matumizi ya vivumishi vya Luganda na Kiswahili sanifu. Data ilichunguzwa maktabani. Utafiti huu unapendekezwa utafi huu vilevile kufanywa nyanjani ili kuweza kubaini jinsi kanuni hizi zinavyotumika kukuza usanifu ama jinsi kanuni za L1 ambayo ni Luganda ama lugha nyinginezo zinavyochangia katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu kutokana na uwiano wa matumizi ya kanuni za kimofosintaksia. Aidha, utafiti huu mwingine unaweza kufanywa kutambua kanuni zaidi ya hizi zilizochanganuliwa katika Makala haya ama katika lugha nyinginezo zenye mnasaba mmoja au tofauti kwa ajili ya kukuza usanif katika matumizi ya lugha za nasaba moja.

**MAREJELEO**


**A**budonia, R. A. (2014). The Syntax of Luganda Adjectives: Katika *Egyptian Journal of Linguistics and Translation*, *1*(1), 35–44.

Abdallah, S. S. (2018). *Uwiano na Utofauti wa Kiisimu Kati ya Kiswahili cha Paje na Makunduchi* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria, Tanzania).

Baertlein, E na Ssekitto, M. (2014) "Luganda Nouns: Inflectional Morphology and Tests," *Linguistic Portfolios*: Vol. 3, Article 3.

Balagadde, R. S. (2016). The Structured Compact Tag-Set for Luganda. *International Journal on Natural Language Computing (IJNLC) Vol*, *5*.

Barno, C . (2013). Muundo wa Kimofo-sintaksia wa Kitenzi cha Kinandi kwa Mtazamo wa Kiunzi cha Kanuni Finyu. *Nordic Journal of African Studies 22(4): 213-235.*, *4*(22), 213-235.

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Macmillan Aidan Ltd.

Chepkwony, L. C. (2012).

Chesswas, J., D (1967). *The Essentials of Luganda*. Oxford University Press, UK.

Chipeta, D 2016. The analysis of Kisukuma determiner in its sentential aspect. Iringa: Ruaha Catholic University (MA dissertation).

Chomi, E. (2013) *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam; Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Chomsky, N. (1981). Lectures on government and binding. Dordrecht: Foris.-. 1986. Knowledge of language: Its nature, origin, and use. *New York: Praeger..(1993)" A Minimalist Program for Linguistic Theory". Kenneth Hale and Samuel J. Keyser, Eds. The View from Building*, *20*, 1–52.

Dixon, R. M. W. (2010). *Where have all the adjectives gone?: and other essays in semantics and syntax* (Vol. 107). Walter de Gruyter.

Egara, M. B. (2016). *Mofosintaksia ya Yambwa katika Kishazi cha* Kiswahili (Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya).

Faki Juma, B. I. K. O. M. B. O. (2019). *Kirai nomino katika kipemba: uchanganuzi wa kimuundo* (doctoral dissertation, suza).

Ferrari-Bridgers, F. (2008). A unified syntactic analysis of Italian and Luganda nouns. *The Bantu-Romance Connection*, 239-258.

Gibson, H., & Guérois, R. (2019). Variation in Bantu copula. *The grammar of copulas across languages*, *73*, 213.

Gromova, N. V. (2008). Maswali Machache ya Usanifishaji wa Kiswahili (Jingine au Lingine?). In *Swahili Forum* (15), 115-120.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers Ltd.

Hyman, L. M., na Katamba, F. X. (2001). November, 2001 The Word in Luganda Larry

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

M. Hyman. *Word Journal Of The International Linguistic Association*, (L)

Iori, I. (2015). *What can the Research on Japanese Anaphoric Demonstratives Contribute to General Linguistics?* Hitotsubashi University.

Jerro, K. (2018). Linguistic complexity : A case study from Swahili. *African linguistics on the prairie*, 3(2), 3–19. https://doi.org/10.5281/zenodo.1251708

Katamba, F., & Stonham, J. (2006). Morphology. NY.

Katamba, F. (2003). Nominal Morphology. In Derek Nurse, Gérard Philippson (eds.) The Bantu languages, Routledge., 103–120.

Katamba, F. (2003). Bantu nominal morphology. *The Bantu languages*, *103*, 120.

Kemuma, W. (2022). Kubainisha Kanuni na Sheria Zinazotawala Muundo wa Maneno katika Sentensi Sahili ya Ekegusii. *Editon Consortium Journal of Kiswahili*, *4*(1), 374-398.

Kitsao, R (2015). Uchanganuzi wa makosa ya kisarufi katika insha za Wanafunzi wa shule za msingi na yanavyochangia Matokeo mabaya ya mitihani, kata ya ganze , kaunti Ya kilifi, Kenya. *Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Pwani*.

Kiyinikibi, N. D. (2021). *The locative in Luganda: a syntax-interfaces approach* (Doctoral dissertation, Stellenbosch: Stellenbosch University).

Kisakwah, B. A. (2014a). *Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili sanifu na za Kisuba*. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Koech, L. C. (2013). *Sintaksia ya kijalizo cha Kiswahili Sanifu: mtazamo wa x-baa* (Doctoral dissertation, University of Nairobi,).

Leah, S na Sseguya, F.N. (2015). *A Luganda grammar*. Yiga Olu-ganda. http://learn-luganda.com.

Lewis, M. P. (2009). *Ethnologue: Languages of the world*. SIL international.

Lusekelo, A. (2009). The structure of the Nyakyusa noun phrase.

Lusekelo, A. (2017). The Swahili noun phrase in its Sentential: Katika *Mkwawa Journal of*

*Education and Development, Juzuu 1, Issue 1,*

Mulei, M., Ambuyo, B., na Nanyama, D. (2021). Mwingiliano wa Kanuni za Kimofosintaksia wa Ngeli Nomino za Luganda Katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu. *Jarida la idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za kiafrika Chuo Kikuu cha Moi, Kenya*.

Massamba, D. P. B, Kihore, Y. M., na Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili*

*(SAMIKISA)*. Sekondari na Vyuo. TUKI.

Massamba, D. P. B, Kihore, Y. M., na Hokororo, J. I.(2012). Misingi ya Fonolojia. Dar es Salaam: TATAKI.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili origins and the Bantu divergence-convergence theory* (No. 48). Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.

Mbaabu, I (1992): *Sarufi ya Kiswahili*: Longman Kenya

Mbwillow, S. N. (2017). Muundo wa Vitenzi, Vivumishi, Vibainishi, Numerali/Namba na

Vielezi katika Kiswahili, 1–26.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1206

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu.Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*.

Longhorn Publishers Ltd, Kenya.

Mwihaki, A. (2007). Minimalist approach to Kiswahili syntax. *Kiswahili*, *70*, 17-40.

Mulei, M. (2014). *Uchanganuzi wa Athari za Kigisu katika Lugha ya Mazungumzokwa Kiswahili,*

*Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Mbale, Nchini Uganda.* Chuo Kikuu cha Uislamu, Uganda.

Ndomba, R. (2006). *Samatengo noun phrase structure. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha*

Dar es Salaam, Tanzania

Nicolle, S. (2007). Metarepresentational demonstratives in Digo. *Interpreting utterances: Pragmatics and its interfaces. Oslo: Novus*, 127-146.

Nyanda, J. (2015). *Athari za Lugha ya Kinyamwezi Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili.* The Open University Of Tanzania.

Obara, J. M. (2014). *Uchanganuzi wa Makosa Yanayofanywa na Wanafunzi Wazungumzaji wa Lugha ya Ekegusii*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Oduor, C., Inyani, K. S., na Kobia, M. J. (2017). Athari za uhamishaji wa sarufi ya Kiluo kwenye upatanisho wa sarufi ya Kiswahili. *Kiswahili*, *76*(1).

Oichoe, M. P. (2005). *Ulinganishi wa kirai tenzi cha Kiswahili na Ekegusii kimofosintaksia: mtazamo wa uminimalisti*. Tasnifu ya Uzamili-Haijachapishwa, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Onyango, V. O. (2018). *Daftari la Isimujamii Kwa Shule za Upili na Vyuo*. (A. B. P. Limited, Ed.) (Tolea la k). Kenya: Susmo Enterprises.

Philipo, Z. T. (2017). Tofauti Baina ya Vivumishi na Viambishi katika Lugha ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, *13*(1).

Radford, A. (1997). *Syntactic theory and the structure of English: A minimalist approach*. Cambridge University Press.

Rijkhoff, J. N. M. (1986). Word order universals revisited: The principle of head proximity. *Belgian Journal of Linguistics* 1. 95-125.

Rizzi, L. (1997). The fine structure of the left periphery. In *Elements of grammar* (pp. 281-337). Springer, Dordrecht.

Rugemalira, J. M. (2007). The structure of the Bantu noun phrase.

Van de Velde, M. (2005). The order of noun and demonstrative in Bantu. *Studies in African comparative linguistics with special focus on Bantu and Mande*, 425-441.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.